JARIDA MAALUMU LA MTANDAONI TOLEO LA KWANZA www.owm.go.tz JANUARI 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.
www.owm.go.tz





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa halfa ya chakula cha mchana pamoja na washiriki wa zoezi la uokoaji wa ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa eneo la Kariakoo leo tarehe 30 Januari, 2025 Ikulu Jijini Dar es Salaam.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itaimarisha mifumo ya usimamizi wa maafa na kuhakikisha tunakuwa na utayari wa kukabiliana na dharura wakati wote.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo katika hafla ya chakula cha mchana pamoja na washiriki wa zoezi la utafutaji na uokozi wa ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa eneo la Kariakoo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa wakati alipotembelea eneo la ajali mwezi Novemba, 2024.

Aidha, Rais Dkt. Samia ametumia hafla hiyo kuwashukuru wote waliojitolea katika zoezi la utafutaji na uokozi na amerejea msisitizo wake kuwa taarifa ya Kamati ya Uchunguzi wa ajali ya jengo kuporomoka Kariakoo itakapokamilika itawekwa wazi.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia ameridhia mwaliko wa Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kariakoo kufanya ziara katika eneo hilo la biashara kwa lengo la kuzungumza na wafanyabiashara wa eneo hilo.

Akijibu mwaliko kutembelea Kariakoo, Rais Dkt. Samia amesema atatumia ziara hiyo pia kuzindua ukarabati wa jengo la Soko Kuu la Kariakoo huku akirejea azma ya Serikali kulifanya soko la Kariakoo kufanya biashara kwa masaa 24.



# Dkt. Biteko Akagua ujenzi Ofisi ya Waziri Mkuu, na Nishati Mji wa Serikali Mtumba




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amefanya ziara katika Mji wa Serikali, Mtumba na kukagua maendeleo ya ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu pamoja na Wizara ya Nishati ambapo ujenzi wa majengo hayo umekamilika kwa asilimia 88.

Akizungumza mara baada ya kukagua na kupata maelezo ya wataalam na wasimamizi wa majengo hayo, Naibu Waziri Mkuu Dkt. Biteko amewapongeza wakandarasi kwa hatua iliyofikiwa na kuagiza majengo yakamilishwe kabla ya mwezi Aprili, 2025.

Aidha, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Biteko ametoa maelekezo kwa mkandarasi ambaye ni Shirika la Nyumba la Taifa NHC kuharakisha kukamilisha Jengo la Wizara ya Nishati ili lianze kutumika kabla ya mwezi Aprili, mwaka huu.

"Serikali chini ya Rais Samia imefanya kazi kubwa, tayari imetoa zaidi ya asilimia 90 ya malipo kwa wakandarasi kwa maana ya kwamba ni kiasi kikubwa zaidi ya ukamilifu wa jengo, najua SUMA JKT mkifanya kwa operesheni mnaweza kukamilisha ujenzi wa jengo hili hata kabla ya muda uliopangwa" amesema Dkt. Biteko

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Nderiananga amemshukuru Naibu Waziri Mkuu kwa maelekezo yake na kusema Ofisi itaendelea kusimamia kwa karibu ili kuhakikisha malengo yanafikiwa kama ilivyopangwa.

"Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Mhe. William Lukuvi namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa ziara hii ambayo ni chagizo kwetu kuhakikisha kwamba ujenzi wa majengo haya unakamilika kwa wakati kama walivyoomba wakandarasi, kwa kuwa sisi ni waratibu inabidi tuwe mfano kwa wengine" amesema Mhe. Ummy.









MATUKIO KATIKA PICHA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, ( Sera, Bunge na Uratibu ) Mhe. William Lukuvi akiwa katika Mkutano wa 18 wa Bunge

# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI Yakagua utekelezaji wa afua za UKIMWI Njombe



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imeelekeza Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu pamoja na Asasi zinazojihusisha na Masuala ya mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI kuhakikisha inaendelea na jitihada za kupunguza maambukizi ya VVU Mkoani Njombe.

Kauli hiyo imetolewa Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Dkt Elibariki Kingu wakati Kamati hiyo ilipotembelea Kituo cha Afya cha Njombe Mjini kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa lengo la kujionea huduma zinazotolewa katika kituo hicho ikiwemo huduma za upimaji UKIMWI, pamoja na kutembelea Shirika lisilo la kiserikali "COCODA" linalohudumia watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Aidha taarifa ya hali ya Mambukizi ya Virusi vya UKIMWI Mkoani humo imeeleza kuwa Mkoa una takribani watu 66,979 wanaoishi na Virusi vya UKIMWI huku jitihada mbalimbali zikiendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na ugawaji wa kondomu.

Kwa upande wake Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga, ametoa shukrani kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge, huku akieleza kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na wadau kukabiliana na kupunguza ongezeko kubwa ya maambukizi ya VVU kwa vijana.



# Naibu Waziri Ummy Afungua kongamano la Global Biosafety



Kongamano hili limeandaliwa na Chama cha Wataaluma wa Ulinzi na Usalama wa Vimelea nchini Tanzania (TaBSA) kwa kushirikiana na Chama cha Kimataifa cha Ulinzi na Usalama wa Vimelea (IFBA).

Kauli Mbiu katika Kongamano hilo ni "Sauti ya Kimataifa: Kuadhimisha Ulinzi na Usalama wa Anuwai za Vimelea Hatarishi"

Aidha Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Menejimenti ya Maafa Sehemu ya Afya Moja inasimamia utekelezaji wa shughuli zote za Afya Moja, zinazojumuisha ulinzi na usalama wa vimelea nchini kwa kushirikiana na wadau.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga amefungua mkutano wa Kimataifa na Kongamano la Kitaaluma (Global Biosafety Conference).

Kongamano hilo limefunguliwa leo katika Ukumbi wa Mount Meru Jijini Arusha lililokutanisha wataalam wa Uwandani wanaoshughulika na Vimelea (Pathogens and Toxins) hatarishi kutoka Bara la Amerika, Ulaya, Asia, na Afrika unaofadhiliwa na Canada's 2025 Weapons Threat Reduction Program.



# Kongamano la kujenga uelewa wa masuala ya VVU na UKIMWI lafanyika Mkoani Njombe







Mkuu wa wilaya ya Wanging'ombe, Mhe. Zakaria Mwansasu, amemuakilisha Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka, katika kuongoza kongamano la kuwajengea uelewa wa masuala ya VVU na UKIMWI, kwa vijana balehe wa shule za Msingi na Sekondari pia amekata keki akishirikiana na wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TACAIDS ikiwa ni ishara ya kusheherekea siku ya kuzaliwa kwa Mhe. Rais, Dkt, Samia Suluhu Hassan leo tarehe 27/01/2025 katika ukumbi wa Johnson Hall Mkoani Njombe

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.





KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480